# OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI
# HALMASHAURI YA BUTIAMA

**Mawasiliano**

- **Mkuu wa Shule:** 0713 600 301
- **Makamu Mkuu wa Shule:** 0764 331 182
- **Mtaaluma:** 0746 439 632

Bumaswa Sekondari
S.L.P 1285
Butiama
…………………

Kumb.Na.BSS/STF/F.17/J.19/2026

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI……………………………………………**

**…………………………………**

**………………………………..**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUMASWA WILAYANI BUTIAMA MKOANI MARA MWAKA …………..**

Nina furaha kubwa kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na **KIDATO CHA TANO** katika shule ya sekondari **BUMASWA** mwaka…………… na utasoma tahasusi ………..

Shule ya sekondari Bumaswa ipo katika Kijiji cha Masurura kitongoji cha Bumaswa umbali wa kilomita zipatazo 30 kutoka Butiama Mjini.Kufika shuleni utatakiwa kupita katika barabara kuu ilekeayo mji wa Mugumu. Ambapo ukifika stendi ya Makutano (Ziroziro) chukua magari yaelekeayo Kiagata au Mugumu, utakuja na gari hiyo hiyo moja na uombe wakushushe katika kibao cha shule ya Sekondari Bumaswa, shule iko Barabara kuu ukishuka kibao cha shule njia ya kuingia shuleni itakuelekeza.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe ………….. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe …………… kuanzia saa 1:00 Asubuhi, mwisho wa kuripoti ni 11:00 jioni na mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………..

**2. MICHANGO YA SHULE (TAREHE YA KURIPOTI**

Fedha zote zilipwe kupitia akaunti NO 30302301014 NMB **Jina** BUMASWA SEKONDARI

Michango mbalimbali

| Na | Maelezo ya Mchango | Kiasi (TSH) |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari (Caution Money) | 5,000/= |
| 3 | Fedha ya kitambulisho na picha | 5,000/= |
| 4 | Fedha kwa ajili ya nembo ya shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

<u>**MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI**</u>

1. Godoro 1 (futi 3), Shuka 3 (2 pink, 1 blue), na Foronya 2.
2. Ndoo 2 (lita 10 na lita 20), Dish moja, na Kidumu cha lita 5 cha maji ya kunywa.
3. Vyombo vya chakula (Sahani ya mfupa, bakuli, kikombe, kijiko).
4. Taa ndogo ya solar (lazima kwa ajili yadharura ya kukatika kwa umeme).
5. Ream paper 2 (A4) aina ya Double A.
6. Madaftari ya kutosha kuanzia 15 ambayo ni Quire Two/Three.
7. Vifaa vya usafi: Hard bloom, fyekeo, jembe na mpini, na Mfagio wa chelewa.
8. Kanga/Kitenge jozi mbili kwa matumizi binafsi.
9. Toilet paper (05) kwa kwa kila mwanafunzi.Dawa za meno na miswaki miwili (02), dawa ya viatu nyeusi.
10. Taulo za kike (pedi) kwa wasichana.
11. Shuka pea moja ya rangi ya pinki kwa wasichana na Blanketi moja kwa wote.
12. Neti moja (01) rangi nyeupe.
13. Ndoo mbili (02) za lita 20 kila moja za rangi ya Blue kwa wasichana na rangi nyekundu/pinki kwa wavulana, Galoni moja (01) ya lita tano (05) kwa ajili ya maji ya kunywa pia awe na ndoo ya lita 10 kwa ajili ya usafi binafsi.

NB: Ndoo moja ya lita 20 itatumika kwa matumizi ya jiko tu.

14. Roka la chuma/ mbao kwa ajili ya kuhifadhia mali zake.
15. Toilet paper tano(5).
16. Sabuni za kuogea na kufulia.
17. Dawa za meno na miswaki miwili (02), dawa ya viatu nyeusi.

**TANBIHI:** Mwanafunzi ataondolewa Bwenini pindi atakapobainika kuwa na vifaa ambavyo hajaelekezwa katika fomu hii. Pia mwanafunzi anatakiwa kuwa na roka moja tu.


<u>**4. SARE ZA SHULE**</u>

**Mashati:** Mashati 2 ya tetron meupe, mikono mirefu.
**Tai:** Tai ndefu ya rangi ya **Dark Blue**
**Sketi:** Sketi 2 za rangi ya **DARK BLUE** (zenye malinda 6), kitambaa kizito, ndefu za kufunika kisigino cha mguu kwa ajili ya darasani,



**Tsheti:** utakuwa na tisheti maalumu za rangi Dark Blue kutumia darasani ambazo zitapatikana shuleni kwa bei ya Tsh. 12,000/= tu.

**Gauni:** Gauni mbili za rangi ya **Kijani jeshi** za solo zinazofunika vifundo vya miguu kwa ajili ya kushindia baada ya masomo



**Viatu:** Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba (visigino vifupi) na soksi ndefu nyeupe(stocking).

**Sweta:** Sweta la rangi ya Dark Blue mikono mirefu.

**Michezo:** Tracksuit rangi ya Blue, raba nyeupe, na t-shirt Blue yenye michirizi.

**Wanafunzi wa Dini ya Kiislam:** Hijabu ya rangi **NYEUPE** (darasani) na **Dark Blue** (nje ya darasa).

5. **MATIBABU**
   - Gharama za matibabu pamoja na nauli kwenda na kurudi nyumbani ni jukumu la mzazi/mlezi wa mwanafunzi.
   - Tunashauri mzazi kumkatia mwanao bima ya afya, au aje na Tsh. 50,400/= kwa ajili ya kukatiwa Bima shuleni.
6. **SHERIA, KANUNI NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Hivyo ni muhimu kwa mzazi kumkumbusha mwanao ajue umuhimu wa nafasi hii. Ni kweli usiopingika kwamba malezi ya wanafunzi kitaaluma , kiroho na kimwili yanategemea ushirikiano kati ya walimu na wazazi.

Mzazi huna budi kumkumbusha mwanao ajue fika kwamba shuleni ni mahala pa kupata Elimu na sio mahali pa kufanya starehe na vioja. Ukosefu wa mawasiliano kati ya pande mbili katika kumuendeleza mwanafunzi kitaaluma daima huzaa wahitimu wasio na ELIMU/UJUZI. Uongozi wa shule umeona ni vizuri kuwashirikisha wazazi katika malezi ya watoto wao hasa katika kuelewa sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za jumuiya ya Shule ya Sekondari BUMASWA. Hivyo hapa shule inakupatia sheria za shule uzisome kwa makini na kuzielewa. Aidha mwanao inambidi kuzisoma na kukiri mbele yako kuwa yupo tayari kuzitekeleza.

Mwisho, baada ya kusoma wewe mzazi/mlezi unaombwa kuweka jina na sahihi pamoja na mtoto wako aweke jina na sahihi akiahidi kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na atapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

A. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
B. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule nimuhimu.
C. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
D. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shulehii.
E. Kutunza usafi wa mwili na mazingira yashule.
F. Kutunza mali binafsi, ya mtu mwingine na mali ya umma
G. Kuvaa sare ya shule wakati wote.
H. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

I. Kila mwanafunzi lazima ahudhurie “**Pared Ground**” kila siku asubuhi na jioni(muda wa kutawanyika). Mwanafunzi asiyehudhuria sehemu hizo atahesabika mtoro na ataadhibiwa.

## MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele; Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira yashule.
xiv. Kudharau Bendera yaTaifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xvi. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

**NB:**

A. **Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki simu, line ya simu na redio; akikutwa navyo atachukuliwa hatua za kinidhamu.**
B. **Haturuhusu mwanafunzi kutembelewa na watu wasiofahamika.**
C. **Mwanafunzi ataruhusiwa kusali katika dhehebu lake shuleni kwa utaratibu wa dhehebu lake kwa kuzingatia sheria za shule.**

- **ADHABU:**

**Mwanafunzi atakayekiuka utaratibu huu atasimamishwa masomo (Suspension) na endapo atarudia atafukuzwa shule kabisa.**

- **MIPAKA**

**I.** Mwanafunzi anapofika shuleni haruhusiwi kwenda nje ya shule bila ruhusa ya **MKUU WA SHULE.**
II. Ni marufuku mwanafunzi kutembelea nyumba za walimu/wafanyakazi au kutoka nje ya shule muda wa masomo bila ruhusa maalumu.
III. Mwanafunzi atatoka nje ya shule kwa kutumia fomu maalumu iliyotolewa na **MKUU WA SHULE.**
IV. Mwanafunzi atakayevunja sheria hii akaenda nje ya shule(kutoroka masomo) bila ruhusa adhabu yake ni **KUFUKUZWA SHULE.**

7. **MAWASILIANO YA VIONGOZI**

- **Mkuu wa Shule:** 0713 600 301
- **Makamu Mkuu wa Shule:** 0764 331 182

- **Mtaaluma:** 0746 439 632
- **Matroni/Mlezi  Bweni:** 0788 291 437

## 8. FOMU MBALIMBALI

# SHULE YA SEKONDARI BUMASWA

### FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINAKAMILILAMWANAFUNZI:________________________________________
2. TAREHEYAKUZALIWA:_________KABILA____________DINI_____________
3. SHULE  YA MSINGI ALIYOTOKA:_____________________________
4. NAMBA YA MTIHANI(PS): _______________________________________
5. MWANAFUNZI ANATOKA MTAA WA/KIJIJI CHA_______________
6. KATA YA:________________TARAFA YA____________________
7. WILAYA YA_________________MKOA WA:__________________
8. URAIA:- MTANZANIA/SIO MTANZANIA ___________________________
9. WAZAZI WOTE WAPO HAI/MMOJA YU-HAI/YATIMA (FUTA ISIYOHUSIKA)
10. JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI_____________________________
11. KAZI YA MZAZI/MLEZI______________KAMA MLEZI TAJA UHUSIANO____
12. ANUANI YA MZAZI/MLEZI_________________SIMU__________

**AHADI YA MWANAFUNZI:**

MIMI _________________________________ Nimesoma na kuyaelewa maelezo ya kujiunga na shule ya sekondari Bumaswa:

(a) Nimekubali nafasi niliyopewa na kuwa nitafuata sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Sheria zote na kanuni za shule nimezisoma na kuzielewa.
(b) Nitahakikisha na ninaahidi kuhudhuria darasani siku zote za masomo.
(c) Nitahakikisha nasoma kwa bidii na maarifa. Sitashiriki katika vurugu za aina yoyote ile pindi nikiwa mwanafunzi hapa BUMASWA sekondari. Naahidi nitadumisha nidhamu nzuri hapa shuleni.
(d) Sitakuwa tayari kudhalilisha shule yangu.
(e) Nitakubali kuchukuliwa hatua stahiki endapo nitakapoenda kinyume na sheria za shule.

---------------------------------        --------------------------------

**JINA LA MWANAFUNZI** **TAREHE**

**SHULE YA SEKONDARI BUMASWA**
**FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MZAZI/MLEZI**

1. JINAKAMILI LA MZAZI/MLEZI:________________________________________

2. TAREHEYAKUZALIWA:______________KABILA___________DINI____________

3. KAZI YA MZAZI/MLEZI ______________________________________________

4. ANUANI YA MZAZI/MLEZI S.L.P ____________________________________

5. SIMU YA MKONONI YA MZAZI/MLEZI ________________YA KAZINI_______________

## AHADI YA MZAZI/MLEZI

MIMI ___________________MZAZI/MLEZI WA MWANA___________Nimesoma na kuyaelewa maelekezo na sheria za shule ya sekondari BUMASWA aliyopewa mwanangu na ninakubaliana nayo.

(a) Ninakubali nafasi aliyopewa mwanangu.
(b) Nitahakikisha kuwa mwanangu anapata mahitaji yake yote muhimu ya shule.
(c) Nitakuwa bega kwa bega na walimu katika kuhakikisha kuwa mwanangu anafuata sheria na kanuni zilizo shuleni. Ni dhamu nzuri ya mtoto ndiyo mafanikio yake.
(d) Naahidi kuwa mwanangu hatashiriki mgomo,fujo na wala makosa ya jinai kama yeye mwenyewe alivyoahidi. Ikitokea akikiuka hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.
(e) Tafadhali jaza majina, namba za simu na kuonyesha uhusiano uliopo kati ya ndugu/jamaa na mwanafunzi watakaokuja shuleni kumtembelea au kuwasiliana nae kwa njia ya simu kupitia uongozi wa shule.

| S / N | JINA | UHUSIANO | NA. SIMU | ANAKOISHI | KAZI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

------------------------------ ------------------------------
**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI** **TAREHE**

**NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI ………………………………………..**


**A: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

BUMASWA DAY SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 1285,
**MUSOMA.**
02/06/2026

The Medical Officer,
……………………………..
……………………………..
………………………………

**RE: …………………………………………… (Full name of student).**
Please kindly examine the above named as to his/her Physical and mental for enrolment as a student, the examination should include the following categories.

1. (a)Eye–Sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech (e) Venereal diseases (f) Leprosy (g) Epilepsy.
2. Neurosis.
3. Pregnancy.
4. Other serious diseases.



**ALFRED ARCHARD RUGEBANDIZA**
**THE HEADMASTER**

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a government Medical Officer)

I have examined the above named person and consider that he/she is physically FIT/UNFIT and mentally FIT/UNIFIT for fulltime of schooling.

1. (a)Eye–Sight………………………………………………………
   (b) Hearing……………………………………………………
   (c)Limbs……………………………………………………
   (d)Speech……………………………………………………
   (e)Venereal diseases……………………………………………………
   (f)Leprosy……………………………………………………
   (g)Epilepsy……………………………………………………
2. Neuroses…………………………………………………………………
3. Pregnancy……………………………………………………………
4. Other serious diseases……………………………………………

**Date ………………………………. Signature …………………….. Station …………………. Designation …………………**